Ninafuatiliwa!

Huwa bado nakuwa ndotoni pale simu yaku inaponiamsha. Oh-ni tayari saa 11:15 ahsubuhi! Nalekea bafuni, nachukua simu yangu kupitia vichwa vikuu vya habari. Mara simu inaita. Dereva wa studio yupo getini kunichukua kuelekea kazini.

Njiani napitia ukurasa wangu wa Facebook WhatsApp kuona ni habari gani motomoto zimepashwa mda huu wa asubuhi. Hili hunipa uelewa mzuri wa namna ya kuanza kipindi baadae. Naingia katika mfumo binafsi wa kuwepo kazini saa 11:40 asubuhi. Haraka naelekea kwenye chumba cha habari na kuwasha kompyuta. Kwenye chumba cha FM nawasalimu wasikilizaji na kuweka ibada ya ahsubuhi kwenye orodha ya matangazo. Kwenye chumba cha habari napitia vichwa vya habari vya IPP – je haya nayoyaona yanawezaje kutokea? Ni vyema kuwa na hakika ya taarifa hizi kabla ya kuziweka kwenye habari zetu za 'Dira'. Lakini nani atanisaidia kuhakiki taarifa hizi?

Inabidi nirudi kwenye chumba cha matangazo ya moja kwa moja kuona "Deutsche Welle news" kupitia satellite channel kwa ajili ya wasikilizaji wetu. Lakini je? Nani atanipa uhakika kuhusu habari hii mahususi? Inanibidi kutumia Kompyuta yangu kupitia kurasa za kijamii. Hakuna jibu. Labda mtandao wa "google" unaweza kunisaidia! Mara napata taarifa inayoshabihiana kidogo na ninayotafuta, japo ni ya zamani kidogo. Nampigia mwanahabari mwenzetu kutoka eneo husika. Akiwa katika hali ya usingizi anapokea simu. "Je umesoma taarifa kuhusu jambo lililotokea katika eneo ulilopo?" Nilimuuliza. "Bado! Ila nitaelekea huko kuandika taarifa ambayo nitakutumia pamoja na sauti za watu waliohusika!" "Ikiwezekana tumia pia ya ofisa wa polisi" Namwambia.

Ni karibia saa 1:30 ahsubuh. Napitia tena habari nyingine na kuziweka kwenye orodha ya matangazo mara baada ya kipindi cha "dira". Sasa inanibidi nizingatie kwa ukaribu habari na mpangilio wake ambapo kwa sasa nimekaribia kusahau kile nilichosoma kwenye habari za IPP.

Katika mda huu, fundi mitambo alikua nakagua mitambo yetu ya urushaji matangazo. Yote imeunganisha kupitia mtandao wa ndani. Alikua akiangalia telemetry data kuona kama mitambo yote ya urushaji matangazo inafaya kazi vizuri. Ili kuwa na hakika zaidi fundi mitambo husikiliza matangazo kupitia redio ndogo ambayo imeunganishwa na simu kwenye sehemu mahususi ya kusilikizia katika mtambo wa kurusha matangazo ili kuhakisha hakuna muingiliano wa matangazo na kituo kingine chochote. Yeye huhakikisha kuwa njia zote za DSL katika studio zinafanya kazi na matangazo ya moja kwa moja yanayoendelea yanakuwa yakirekodiwa. Ilibidi pia aziwashe kompyuta 20 kwa mara nyingine katika studio kwa sababu zimesasishwa usiku uliopita.

Baada ya hapo akaenda kwenye ukurasa wetu katika mtandao na kuweka mada mpya kwa kuisasisha ile niliyompa jana na kuweka kamera tayari. Leo tunataka kurusha matangazo ya moja kwa moja ya mahojiano na mgeni wetu maalumu katika kipindi cha “Basket morning”. Tuna hakika kuwa wengi wa wasikilizaji wetu watapenda kumuona katika YouTube pamoja na baadhi ya mambo tuliyoandaa.

Sasa napitia jumbe fupi za maoni ya wasikilizaji wetu kwa DW na taarifa zetu. Kabla sijazisoma, napitia orodha ya IP ya wasikilizaji wetu wa matangazo ya moja kwa moja katika mtandao na maeneo wanaposikiliza. “Ni furaha kwangu kuwasalimu wasilikilizaji wetu nchini Norway, Marekani, Switzerland (Geniva) na wengi kutoka China leo! Pole kwao kwa kuwa hawaruhusiwi kuja nyumbani leo kwa sababu ya ugonjwa wa virusi vya Corona! Ninaaza kuongea na wasikilizaji wetu na kusoma maoni yao katika jumba fupi. Alafu nasikia sauti za ngoma za PFL ya habari TBC na nawaunga TBC hewani. Inabidi niweke matangazo (commercials) yasiyo fanana kwenye orodha. Lakini sasa msomaji habari wa TBC anaeleza kuhusu ile habari niliyoiona kwenye kwenye ukurasa wa ITV. Nani mwinginea angeweza kunipa hakika ya hiyo habari? Napokea simu kutoka kwa mwahahabari wetu wa nje. “Niliweza kumhoji inspeckta wa polisi!” Aliniambia. Nitakutumia taarifa na mahojiano haya”. Jinsi again nimefurahishwa na mwenzangu huyu. Kweli yeye huwa mahali sahihi pale anapohitajika jambo litokeapo”

Lakini sasa mgeni wetu leo anaingina studio. Nilimfuata kwa kamera yangu iliyokuwa nje ya jingo la studio na kumsalimu alipokua akipanda ngazi.

But now our guest of today is entering the studio. I followed him on the CCAM mounted outside the studio building and great him coming up the stairs. Anapokaribishawa studioni, mara moja naanza kupakua kipindi kipya cha “UN Wakkala” , na kupitia kipindi cha “Kwaya ya leo” kilichokwisharekodiwa . Vipindi hivi vitakuwa katika seva yetu ya programu za redio baadae. Sasa matangazo (commercials) yanayorushwa hewani yanakaribia kuisha na napawashwa kuweka kipande cha mziki kupata mda kidogo wa kuongea kuhusu kipindi kifuatacho na mgeni wetu maalumu. “Je ulipata maoni yangu kupitia WhatsApp kuhusu mambo ambayo kipindi cha leo kitahusisha?” “Ndio, asante,” alijibu. Na hasa ile mada ya tatu ni muhimu sana na tunapaswa kutilia mkazo hapa!”

Wakati wote huu, fundi mitambo alikua akijiandaa kuwa tayari kwa mahojiano ya moja kwa moja kwenye YouTube kwa kutumia kamera na Kopyuta (Laptop). “Ndugu msikilizaji, tuna furaha sana kuwa mnaweza kutuangalia leo, kama unafungua ukurasa wetu wetu wa YouTube! Ni rahisi. Kwenye simu yako janja ya mkononi, fungua YouTube na tafuta Sautiyainjili na waweza kutuona pamoja na habari nyinyinezo baadae. Waweza kutuma maoni yako kwa njia ya ujumbe mfupi, kwenye ukurasa wetu wa Facebook na Instagram. Nitayaoma baadae. Pia waweza kutupigia simu mara tu tutakapoanza kumuomba mgeni wetu kujubu maswali yenu baadae….”

Ilikua furaha kwangu kuungana na wasikilizaji wetu kwenye matangazo ya moja kwa moja kutoka TWR, Afrika Kusini, kwa sababu nilitaka kusikia ripoti ya afisa polisi akithibitisha taarifa ya habari ITV:

“Ni kweli” alisema, “popote tuwapo tunatumia teknolojia ya habari na mawasiliano na hatuwezi kuiepuka! Lakini tunaweza kujifunza kuitumia na kuifanya yenye manufaa kila siku!” Hivyo ni vyema kujiandaa kuitumia teknolojia ya habari na mawasiliano kabla haijakutumia!”

Watumishi Radio Sauti ya Injili